Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 14.04.2022; Accepted 18.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M. *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

# Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ya Said A. Mohamed.

**Matthew Kwambai.**
**Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.**
**Email: kwambai09@yahoo.com**

## IKISIRI

Makala haya yanalenga kuangazia matumizi ya jazanda pamoja na uamilifu wake katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ya Said A. Mohamed. Jazanda ni matumizi ya maneno ambayo yana fumbo huku yakitoa taswira ya aina Fulani. Said A. Mohamed ametumia jazanda kwa kazi zake kama *Amezidi* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* imetumia mbinu hii kwa njia ya kipekee. Nadharia iliyotumiwa katika kazi hii ni ya Umuundo ambao unasema kuwa kazi ya fasihi inakuwa na muundo ambao unahusisha fani ambazo zitaweza kutumika katika kuwasilisha ujumbe na hivyo maudhui huwa na uhusiano mkubwa sana na fani zitakazotumiwa kuyawasilisha. Utafiti ulifanywa maktabani kwa kuchambua *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, vitabu tofauti na makala mitandaoni. Nakala hii ilipata matokeo kuwa kichwa cha kitabu hiki ni jazanda, pia, kulikuwa na jazanda ya bahari na yale yaliyokuwa yakifanyika kwenye bahari. Jazanda zote zilizotumika ziliweza kuendeleza maudhui kama vile: Mapenzi miongoni mwa vijana, Ndoa, Elimu, Mahusiano katika familia na jamii, Utamaduni na Dini. Uamilifu wa jazanda ni kudhihirisha jinsi mabadiliko yameathiri vijana na hivyo kwenda kinyume na utamaduni na wazee.

**Maneno Muhimu:** Jazanda, fumbo, taswira, kitendawili.

------------------------------------------------***------------------------------------------------

**How to cite this article in APA.**

Kwambai, M. (2022). Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ya Said A. Mohamed. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 4(1), 399-403. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358

------------------------------------------------***------------------------------------------------



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 14.04.2022; Accepted 18.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M. *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

**UTANGULIZI**

Kazi hii iliangaza jazanda katika tamthilia ya Kitumbua kimeingia mchanga, japo kuna kazi zingine ambazo zimetumia jazanda kama vile *Kusadikika* ya Shaaban Robert (Sangolo, 2009), *Walenisi* na *Mafuta* za Katama Mkangi na *Amezidi* ya Said A. Mohamed, utafiti huu uliona kuwa tamthilia teule ilikuwa na upekee katika matumizi ya jazanda kuwasilisha masuala mbalimbali muhimu. Ni kutokana na upekee huu ambao utafiti ulifanywa kwa kufuata nadharia ya Umuundo na hivyo kugundua jazanda ya kichwa cha Tamthilia na jazanda ya bahari, lengo la jazanda hizi lilikuwa kuwasilisha ujumbe kuhusu mgogoro baina ya ukale na usasa, ukale ukishikiliwa na wazee na usasa ukishikiliwa na vijana.

KKM ni ufupi wa jina la tamthilia *Kitumbua Kimeingia Mchanga*.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Kulingana na Scholes (1974) na (Wafula & Njogu, 2007), nadharia ya Umuundo inaangazia fani na jinsi fani hizo zinachangia kuwasilishwa kwa maudhui katika kazi yoyote ile. Kulingana na nadharia hii, fani na hasa mbinu zinazotumika katika kazi ya sanaa huwa na uamilifu wa kuwezesha maudhui kuwasilishwa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Jazanda Zilizopatikana**

Jazanda kulingana na Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2013), ni picha ya kitu iliyomo kichwani mwa mtu; taswira.

**Jazanda ya Kitumbua Kimeingia Mchanga**

Bi. Haja anatumia jazanda upishi wa kitumbua. Anapika vitumbua na kuviweka mchanga na kisha kuwapa Mwanawe Mambo na familia yake ili kuvila. Anamweleza Mkasa mwanawe Bi. Sikitu, kuwa:

> Dunia tuliyo nayo imebadilika. Nyinyi watoto hata hamjui jinsi ya vyakula vinavyopikwa na vinavyopakuliwa. Hamjui hata vinavyoliwa na visivyoliwa…hata ladha tamu zimekupoteeni! Chapwa kwenu imekolea na chungu imekolea na chungu huwa tamu. Huo nd"o usasa… ndiko mnakokuita kuendelea. (KKM, uk 5)

Haya ni malalamishi ya Bi. Haja, mamake Mambo. Anatoa lawama kwa mwanawe na mke wake. Anasema kuwa kizazi cha mwanawe hakijui chakula kinachofaa kuliwa wala jinsi ya kukipika. Anasema kuwa sababu ya haya yote ni usasa na maendeleo. Bi. Haja analaumu kizazi cha mwanawe, kuwa kizazi hicho ndicho chanzo cha kitumbua kuingia mchanga, anathibitisha msemo kuwa "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Bi. Haja analaumu Mambo na mke wake Bi. Sikitu kuwa tabia za watoto wao na hasa Fikirini ni kutokana na malezi yao mabovu. Anatoa mfano wa kupika kitumbua ambacho kinamtoza mtu jasho, mtu yeyote akitaka kupika kitumbua lazima awe na uelewa ambao unatokana na vizazi vilivyotangulia. Hata hivyo, anasema kuwa kitumbua kinaweza kupikwa vyema, lakini mwisho mtu mwingine asiye na makini na asiyejali aje na kukiweka mchanga na kisha kukulazimisha kuila. Anahitimisha kuwa mtu mwenye akili zake timamu hawezi kukubali kukila kitumbua kilichoingia mchanga.

Kupitia kwa jazanda hii ambayo inatiliwa nguvu na Bi. Haja kupitia kwa upishi wake, ujumbe unawasilisha kwa Mambo na Mke wake Bi. Sikitu, pale wanapokula chakula, Sikitu anasema:

> Kuna neno, kuna neno… kavitia mchanga makusudi kuwasilisha ujumbe kwa lugha ya fumbo. Hiyo ni siri yake mpaka tutakapomwuliza… (KKM, uk 21/22)

Haya ni maneno ya Bi. Sikitu baada ya familia kula vitumbua vilivyokuwa vimewekwa mchanga na bibi yao Bi. Haja. Maneno haya ni hitimisho kwa kila mmoja katika familia ya Bw. Mambo, wanajua kuwa bibi yao alikuwa na ujumbe aliotaka kupitisha kwa kuweka mchanga kwa vitumbua.

Kadri muda unavyosonga, Bi. Haja anaeleza Mambo na Sikitu kwa kejeli na kujifanya kuwa hakuelewa kwamba vitumbua vya awali vilikuwa na mchanga na kuwa



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 14.04.2022; Accepted 18.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M. *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

hakuelewa kuwa vitumbua vilivyo na mchanga haviliki. Anawaeleza wanawe kuwa:

> Na nyinyi ni nani kama si watoto wachanga…mambo yanawaharibikia hivihivi mbele ya macho yenu na bado mnatazama tu. Mmo mnashadidia kutaka kuingiza kitumbua kilichoingia mchanga nyumbani mwenu. (KKM, uk 24)

Maelezo haya yanadhihirisha lawama ya mama kwa kizazi cha watoto wake ambacho hakifuatilia utamaduni na kuacha mambo kuharibika kwa watoto wao huku wakiwa macho. Bi. Haja analaumu Mambo na Sikitu kwa kuacha Fikirini kuchagua mchumba Hidaya, anayeonekana kuacha utamaduni na kufanya mambo ambayo yanaenda kinyume na mila na desturi kwa sababu ya elimu na athari ya usasa. Bi. Haja anafaulu kuwasilisha ujumbe na kuwashawishi wana wake kujaribu kuvunja uchumba wa Fikirini na Hidaya. Wazazi wa Fikirini, wanataka kuendeleza ndoa baina ya Fikirini na Subira kwa sababu walikuwa wamewekeana miadi na ahadi na wazazi wa Subira. Kuna uhusiano wa matukio ya *Kitumbua kimeingia Mchanga* na mawazo ya Rehak (2007) ambaye anaangazia ulinganifu wa *Kichwamaji* na *Mgeni*. Rehak anasema, kuna suala la utengano baina ya kizazi cha vijana na kile cha wazee.

Kuna ukengeushi baina ya Kazimoto na mamake, hii ndiyo sababu Kazimoto anapofika kutoka safari ya kumtembelea rafiki yake, Kamata, hataki kuulizwa maswali na mama yake. Pia, Meursault anakengeushwa kutoka mamake anayempenda, ndiposa anachukua muda mrefu kabla ya kumtembelea. Rehak anasema wahusika hawa wawili wanawapenda mama zao na hii inajitokeza ndani ya migogoro inayodhihirika baina ya mama na wavulana hawa wawili. Hali hii kulingana na Rehak, inakuwa matokeo ya kutokuwa na mawasiliano baina ya wazazi na watoto. Suala hili la kukosa mawasiliano si la familia tu bali jamii kwa ujumla. Rehak anasema kuwa Kazimoto na Meursault wanajipata katika hali mbalimbali ambazo japo wanajaribu kujinasua, ila hawafanikiwi. Mgogoro unaoangaziwa na Rehak (2007) ni sawa na ule unaodhihirishwa na jazanda ya Kitumbua kuingia mchanga.

Lengo la matumizi ya jazanda hii ni kuonyesha lalama za kizazi cha wazee kwa vizazi vinavyofuata kwa kutozingatia utamaduni na maadili yanayotokana na utamaduni huo, hivyo kuharibu kizazi husika kuiletea aila aibu. Kitumbua kinaingia mchanga kwa sababu ya mapuuza ya kizazi cha mzee Mambo na vizazi vinavyofuata, kulingana na mamake Bi. Haja. Mapuuza haya yanatokana na usasa ambao unaambatana na elimu na utamaduni wa kisasa ambao unakubali mambo ya kigeni huku ukiona kama utamaduni wa kale haufai na umepitwa na wakati. Hali hii inazua mgogoro miongoni mwa vizazi hivi viwili kila kimoja kikivuta ngoma upande wake bila kujali upande ule mwingine.

**Jazanda ya Bahari.**

Fikirini anatumia jazanda ya bahari kudhihirisha maisha kama kigeugeu. Anasema kuwa bahari mara nyingine huwa shwari na nyingine huweza kusababisha gharika. Bahari huwa mahali pa kutembelewa kwa kujivinjari na nyakati zingine huogopwa kwa sababu ya kuweza kuwa na mchafuko na kufanya kuwe na gharika litakalosababisha maafa. Fikirini anasema:

> Aaaa, basi tu nafikiri hivyo- mimi naona bahari kama kiumbe; mithili ya jitu kubwa lenye ukubwa usio mwanzo mwanzo wala mwisho. Kama vile jibaba lisilo ukomo wa amri na utawala wa mabavu. (KKM, uk 36)

Jazanda hii ya bahari ambayo inatumiwa na Fikirini katika mazungumzo yake na Faki rafikiye na Mzee Nia inaonyesha jinsi vijana wanavyoona kuwa wanaonewa na wazee. Anadhihirisha kuwa wazee wana mamlaka ambayo wanatumia kimabavu kuwadhulumu na kuwalazimishia mambo mbalimbali yakiwemo utamaduni, ukale na masuala yaliyopitwa na wakati kama kuchaguliwa wachumba. Fikirini anaona kuwa kijana wa kileo ana uhuru wa kuchagua anachokipenda tofauti na alivyokuwa baba yake



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 14.04.2022; Accepted 18.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M. *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

miaka hamsini iliyopita. Kwa kizazi cha wazee, mambo hayafai kufanywa jinsi yanavyofanywa na kizazi cha vijana. Mgongano huu unamfanya Fikirini kulinganisha bahari na yanayotendeka na maisha ya kila siku. Anahitimisha kuwa maisha ya wanyama baharini na yote yanayofanyika baharini ni kigeugeu sawa na maisha ya binadamu yanavyogeuka kila uchao. Sangolo (2009), anatafiti mandhari ya kijazanda katika *Walenisi na Kusadikika*, ambayo aligundua kuwa yalilengwa kuwakilisha masuala kwa njia mpya ambayo ingeepuka uwakilishi wa kawaida wa uhalisia. Jazanda za utafiti huu tofauti na matokeo ya Sangolo, yanalenga kuwasilisha uhalisia wa kijamii na kutoa taswira na ujumbe kwa vizazi tofauti kuhusu mgogoro baina yao na matokeo yake.

Bahari inakuwa na uhai wa kujaa na kupwa, sawa na uhai wa wanyama wengine ambao wanadhulumu wenzao. Wanyama wadogo kama vidagaa vinadhulumiwa na wanyama wakubwa wa majini ilhali havikuomba kuwa baharini bali vilijikuta tu mle baharini. Fikirini anapozungumza na Bw. Nia anasema:

> …papa kumtafuna changu, nduwaro kumtoboa kanadi… pweza kumzonga na kumbomolea makazi yake kaa; mradi moto unawaka baharini; ndani ya matata ya maji, mnazidi matata. Katika hali kama hii vidagaa havina salama wala utulivu. Havikuomba vidagaa kuja duniani wala kuzaliwa baharini. Vimejikuta tu kukabili majaliwa yao. Havikuwa na uchaguzi zamani wala havina uchaguzi sasa. Maana maisha yao yanaongozwa na nguvu zilizomo baharini… mikondo, kasi, pepo zipigazo juu, mawimbi, dhoruba na manyama makubwa. Hata yawe ndio baba; hata yawe mama, kaka au dada hula vizazi vyao… (KKM, uk 38)

Hapa inadhihirika kuwa, kuna mgogoro baharini kutokana na mambo mbalimbali yanayotoka na dhuluma ya wanyama wenye nguvu ambao wanatumia nguvu zao kuwatesa wanyama wadogo ambao walijipata duniani wala hawakuwa na uwezo wa kufanya uchaguzi wa kuwepo au kutokuwepo duniani. Sawa na hali hii maisha ya binadamu katika jamii inakumbwa na mtafaruku unaotokana na utamaduni na mila zinazotekelezwa na kizazi cha wazee kinacholazimisha kizazi cha vijana bila kujali mahitaji na maoni yao yanayotokana na kubadilika kwa mambo kwa sababu ya athari ya elimu, usasa na tamaduni zingine ambazo kizazi hiki changa kimekumbana nazo. Hali inafanywa kuwa mbaya zaidi na hali kwamba mzazi ana mamlaka na uwezo kulingana na tamaduni husika na hivyo, wasemacho vijana hata kiwe na uzuri gani huangukia masikio yasiyotaka kukisikia. Wazee hutaka vijana wafuate watakayosema bila kujali mitazamo yao hata yakiwa yana mashiko.

Uamilifu wa jazanda ya bahari ni malalamishi ya kizazi cha vijana dhidi ya kile cha wazee. Vijana wanasema kuna uonevu mkubwa duniani sababu ya vizazi vilivyotangulia kulazimisha mambo ya kale na utamaduni kwa dunia ya sasa ambayo imebadilishwa na utamaduni wa kimagharibi na elimu ambayo wao kama vijana wamepata. Kipacha (2015), anaangazia taswira ya ndege katika kazi za Shaaban Robert, anagundua kuwa kazi za Shaaban Robert zinasawiri dunia ya ubaguzi na dhuluma ya Mwafrika chini ya mgeni, taswira hii ya ndege inatumiwa na mwandishi kudhihirisha matumaini ya Waafrika kutafuta ustawi wa maisha. Utafiti huu tofauti na wa Kipacha, unaonyesha kutamauka kwa vijana sababu ya msukumo kutoka utamaduni ambao umeshikiliwa na wazee.

Kwa ujumla, jazanda za kitumbua na bahari zimetumika kupitisha ujumbe wa mgogoro uliopo baina ya wazazi kwa upande mmoja na vijana kwa upande mwingine. Wazee wanashikilia utamaduni kwa hofu kuwa huenda watapata aibu ikiwa utamaduni utapotea, wanaona kuwa kitumbua kimeingia mchanga kwani vijana wamefuata usasa bila kujali matokeo yake. Hali hii inawafanya wazee kuwa na mioyo migumu na kuwalazimisha vijana kufuata mila bila ya nafasi ya kuuliza maswali, hawajali mahitaji yao. Matokeo ni vijana kukaidi maagizo na maelekezo. Vijana wanatumia



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.358
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 14.04.2022; Accepted 18.04.2022; Published on 30.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kwambai, M. *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

dawa za kulevya, vileo na kufanya mambo mengi mabaya. Jazanda ya bahari ni malalamishi ya vijana kwa dhuluma za kulazimishiwa kufuata mambo ya kale ambayo kulingana nao yamepitwa na wakati. Jazanda ambazo zimetumika katika tamthilia husika zimeendeleza maudhui kama vile: Mapenzi miongoni mwa vijana, Ndoa, Elimu, Mahusiano katika familia na jamii, Utamaduni na Dini.

Hata hivyo, katika kilele cha matukio kwenye tamthilia, kunakuwa na kinaya kwamba kitumbua kiliingia kwa mchanga kwa Bw. Mambo na ndoa ya Baddi. Bw. Mambo anapatikana na kosa la kuuza dawa za kulevya na ndoa ya kisiri. Mwanawe Baddi anapatikana kwenye njia panda kwa kukubali kuchaguliwa mchumba, kisha wakati wa harusi kitumbua kinaingia mchanga. Kwa upande wa Fikirini na Hidaya, harusi yao inafanikiwa. Dhamira ya mwandishi kwa kutumia jazanda hizi na kudhihirisha kinaya mwishoni ni kuonyesha umuhimu wa kuchagua mazuri ya kale na mazuri ya sasa na kuwe na majadiliano baina ya kizazi cha wazee na kizazi cha vijana ili kuwe na masikizano na utangamano miongoni mwa wanajamii.

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Jazanda za kitumbua na bahari zimefanikiwa kutoa taswira ya mgogoro wa ukale unaoshikiliwa na wazee kwa sababu ya mila na utamaduni na usasa wa vijana unaotokana na elimu na tamaduni za kigeni. Hata hivyo, jazanda hizi zinadhihirisha kuwa wazee wana makosa kwa kiwango Fulani kupitia kwa siri za Bw. Mambo na pia vijana hawafai kukubali utamaduni tu bila ya kuuliza maswali, hii inadhihirika kupitia kwa kitumbua kuingia mchanga kwa harusi ya Baddi na Zawadi. Vijana hawa walikuwa wamekubali kufuata maagizo ya wazazi wao huku Fikirini na Hidaya wakipinga kuchaguliwa wachumba, kilele Fikirini na Hidaya wanafanikiwa katika harusi yao. Jazanda hizi zinatoa ujumbe kuwa ili jamii ifanikiwe lazima izingatie mazuri ya kale na kuyachanganya na mazuri ya sasa.

## MAREJELEO

Bernard, H. R. (2002). *Research Methods in Anthropology: Qualitative and quantitative methods* (3rd edition). AltaMira Press, Walnut Creek.

Kipacha, A. (2015). Taswira za Ndege Katika Maandiko ya Shaaban Robert.: *Swahili Forum* 22, 1-19.

Longhorn Publishing House. (2013). *Kamusi ya karne ya 21*. LPH.

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (1999). *Research methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Act Press.

Rehak, V. (2007). *Kazimoto and Meursault: Brothers in Despair and Loneliness.* CompairingKezilahabi's *Kichwamaji* and Camus *L'Etranger*. *Swahili Forum* 12, 135-151.

Sangolo, J. A. (2009) *Mandhari ya Kinjozi Inayotumika Kumulika Matatizo ya Jamii*: Mfano wa Riwayaza *Kusadikika* na *Walenisi*. Tasnifu ya uzamili chuo kikuu cha Egerton.

Scholes, R. (1974). *Structuralism: An Introduction*. Yale University Press New Haven

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org